

Lugha kama Mfumo wa Maana Matinishi: Mfano wa Uamilifu wa Kanuni Geuzaji katika Matini za Sajili ya Mchezo wa Kandanda

Mark A. Odawo
Chuo Kikuu cha Rongo

Ikisiri

Jukumu la msingi la lugha kama mfumo wa maana unaowakilishwa kwa maumbo ya kisarufi ni kukidhi mahitaji ya mawasiliano mionganii mwa watumiaji wake. Lugha hupata uamilifu huu baada ya vipashio vyake kupangwa na kuhusishwa na kanuni za kimofosintaksia za lugha hiyo. Upangilifu huu ndio unaozalisha matini zenyenye usarufi, ukubalifupi na mshikamano na ambazo hujitosheleza kimaana. Kanuni Geuzaji huamilishwa kimofosintaksia kwa mujibu wa jinsi elementi za tungo zinavyopangwa kwa njia anuwai ili kuzalisha matini husika. Makala hii inachukua mkabala unaoangalia lugha kama mfumo unaotegemea Kanuni Geuzaji ili kuzalisha matini zenyenye maumbo mbalimbali zinazotosheleza mahitaji ya mawasiliano. Kwa hiyo, makala inadadisi jinsi Kanuni Geuzaji inavyoweza kuamilishwa katika kufuma maana matinishi kutokana na matini za sajili ya mchezo wa kandanda.

1.0 Utangulizi

Makala hii imejengwa katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza ina maelezo ya awali kuhusu jukumu la kimsingi la lugha. Mbinu zilizotumiwa kupata data ya utafiti huu zimeelezwa katika sehemu ya pili. Dhana ya maana matinishi imepambanuliwa katika sehemu ya tatu. Kulingana na data ya makala hii, lugha ya matangazo inayotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda inadhihirisha mshikamano wa matini kupitia aina mbalimbali za Kanuni Geuzaji kama ilivyopambanuliwa katika sehemu ya nne. Sehemu ya mwisho inatoa hitimisho la makala hii. Makala hii inaangalia matini kama mfululizo wa usemi au kauli mbalimbali zinazotolewa na watangazaji wa mchezo wa kandanda.

Lugha kama chombo cha kufanikisha mawasiliano mionganii mwa wanadamu, hutumia sauti nasibu na ishara zilizoteuliwa na kukubaliwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za wanajamii wanaohusika (Bolinger na Sears, 1981). Cook (1969) anasema kuwa binadamu hujamiisha na kumilikisha lugha kama mali yao wanapoitumia kwa kufuata kanuni za kimofosintaksia zinazokubalika. Utaratibu huu ndio unaozalisha matini sarifu zenyenye uamilifu kimaana katika miktadha maalumu.

Matumizi ya lugha kimuktadha hutambulika na kubainika pale yanapoongozwa, kuelekezwa na kudhibitiwa na kaida, maadili na mazoea ya jamii

husika. Miktadha hii ndiyo inayozua sajili mbalimbali kutegemea shughuli na mahitaji ya wanajamii. Halliday na Hasan (1989) wanatoa fasili ya sajili kama maneno anayoyatumia mtu kutegemea shughuli aliyomo. Huu ni upambanuzi wa lugha kwa mujibu wa inakotumiwa na inavyotumiwa. Maelezo haya yanahusisha sajili na uamilishaji wa lugha katika miktadha ya jamii. Utafiti huu uliegemea katika upambanuzi wa maana matinishi kama inavyodhihirika katika sajili ya mchezo wa kandanda.

2.0 Mbinu za Utafiti

Mtafiti alihusisha usikilizaji wa kauli za matangazo ya moja kwa moja ya mchezo wa kandanda yanayopeperushwa kwenye vituo vya radio kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Vituo vilivyohusishwa ni *Radio Citizen*, *Radio Jambo*, *Radio Maisha*, *KBC Radio Taifa*, *Q FM* na *Milele FM*. Taarifa zinazohusu mchezo huu kwenye vituo hivyo zilichambuliwa. Aidha, vituo vya runinga vilivyohusishwa katika kutazama taarifa za mchezo wa kandanda ni *Nation Television (NTV)*, *Q Television (Q TV)*, *Kenya Television Network (KTN)*, *Kenya Broadcasting Corporation (KBC)* na *K 24 Television (K 24)*.

Kati ya timu 16 zinazoshiriki ligi kuu ya mchezo wa kandanda nchini Kenya, uchunguzi huu ulishirikisha matangazo ya moja kwa moja ya mechi za timu tano ambazo ni Gor Mahia, AFC Leopards, Tusker, Ulinzi na Sofapaka. Timu hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu ni pinzani na maarufu zaidi kwa kushikilia nafasi za mwanzo katika jedwali la ligi, hasa kuanzia mwaka 2012 hadi 2014. Hali hii imezifanya timu hizi kuwa na wafuasi wengi zaidi wanaopenda kusikiliza matangazo ya mechi zake. Idadi hii inaoana na kiwango cha sampuli cha 30% cha idadi jumuifu kinachopendekezwa na Kothari (2008) kuwa na uwezo wa kuzalisha data yenye tabia sadifu na wakilishi.

Mbinu ya uteuzi wa kimakusudi ilitumiwa pia katika usikilizaji wa matangazo ya mechi zinazohusu timu tano maarufu za Uingereza zilizo na ufuasi mkubwa nchini Kenya. Timu hizo ni Arsenal, Manchester United, Chelsea, Manchester City na Liverpool. Matangazo ya mechi zinazohusisha timu hizi hurushwa moja kwa moja kwenye vituo vya radio vinavyotangaza kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Data iliyotokana na sampuli hii iliweza kudhihirisha tabia na kutoa taarifa zilizonufaisha utafiti huu.

3.0 Maana Matinishi

Kulingana na Halliday (1985), maana matinishi huhusika na kanuni za kisarufi zinazoelekeza matumizi ya lugha kwa lengo la kisarufi ujumbe na kufanikisha mawasiliano. Halliday (1985) anafafanua zaidi kuwa maana matinishi ni mhimili mmojawapo wa Sarufi Amilifu Mfumo (SAM) unaoangalia lugha sawa na mfumo

au mtandao wa maana unaowakilishwa kwa maumbo ya kisarufi. Kwa mtazamo huu, mfumo wa lugha huangaliwa sawa na uamilifu wa maneno.

Halliday (2004) anaeleza kuwa katika kuamilisha tungo, utanbu wa sintaksia unaohimili maana matinishi hujengana na kudhibitiana kwa kiasi kikubwa na tanzu za semantiki na pragmatiki. Hii ina maana kuwa lugha huwa ishara ya kufaulisha mawasiliano pale ambapo pragmatiki hudhibiti semantiki, nayo semantiki ikidhibiti sintaksia. Hivi ndiyo kusema kuwa maana katika lugha hukamilika inapohusishwa na muktadha wa matumizi. Kadhalika, vipashio vya lugha hupata maana pale vinapopangwa kwa kufuata kanuni za lugha husika. Kwa hiyo, maana matinishi huangalia tungo kwa namna ambavyo inakidhi mahitaji ya umilisi mawasiliano, uhalisi wa kisemantiki pamoja na utoshelevu wa kipragmatiki.

Halliday (1985) anaeleza zaidi kuwa maana matinishi inazingatia usarifu na ukubalifu wa sentensi pamoja na mshikamano katika kauli ndefu. Aidha, inahusika na jinsi vipengele vya usemi vinavyounganishwa na vingine ili kuleta mshikamano katika matini. Hii inamaanisha kwamba maana matinishi hutekeleza jukumu la kuunda matini inayoleweka kama ujumbe uliokamilika na wala si vipande vya maneno au vishazi viliviyotengwa. Mwinlaam na Winfred (2016) nao wanasema kuwa maana matinishi hutokana na ufinyanzi wa taarifa zinazopatikana katika viambajengo vya kisintaksia ili kuunda tungo amilifu kwa kufuata sheria za lugha husika. Kwa upande wake Caffarel (2010), anaeleza maana matinishi kama zao la ufumaji wa vipashio vya kisarufi kwa namna inayozalisha tungo ambazo huzingatia muktadha katika kuitisha ujumbe.

Halliday na Hasan (1989) wanaeleza kuwa kuunganishwa huku kwa vipashio mbalimbali ili kuzalisha matini kamilifu na amilifu ndiko kunakorejelewa kama mshikamano wa matini. Wanaendelea kusema kuwa mbali na sintaksia, mshikamano wa matini ni dhana ya kisemantiki inayoelezea ufungamano na uhusiano wa kimaana unaopatikana katika vipashio vya lugha vinavyojenga matini. Vilevile, wanaeleza kwamba mshikamano hutokea ikiwa kufasiriwa kwa kipashio fulani katika usemi au matini kunategemea kipashio kingine kinachofuata au kutangulia katika mpangilio wa kisintaksia.

Ufasiri huu huzingatia matumizi ya lugha kimuktadha pamoja na ufungamano na kaida za mawasiliano. Hii ina maana kwamba maana matinishi humwezesha msemaji kupanga vipashio vya lugha kwa namna inayozalisha usemi unaowasilisha ujumbe kulingana na muktadha. Katika harakati za kuwasiliana na wasikilizaji wao, watangazaji wa mchezo wa kandanda hutumia matini zenye miundo mbalimbali iliyogeuzwa na ambazo hufungamana na muktadha husika. Hii ina maana kuwa lugha inayotumiwa katika matangazo ya sajili ya mchezo wa kandanda inadhihirisha mshikamano wa matini kuitia aina mbalimbali za Kanuni Geuzaji.

4.1 Kanuni Geuzaji

Ugeuzaji ni dhana ya kisintaksia iliyio na msingi wake katika Nadharia Geuzaji/Sarufi Geuza Miundo Zalishi ambayo iliasisiwa na Noam Chomsky katika kitabu chake cha *Syntactic Structures* (1957). Chomsky (1957) anaeleza kanuni geuzaji kama utaratibu wa kubadili maumbo ya maneno kuwa maumbo mengine kwa kufuata sheria maalumu. Anasema zaidi kuwa sarufi geuzaji hujengwa kwenye wazo kwamba katika lugha kuna sentensi ambazo ni za msingi zinazotokana na kaida mahususi na sentensi zingine nyingi zenye maumbo tofauti lakini zenye maana sawa. Kanuni hii hugeuza sentensi kutoka umbo la ndani hadi la nje wakati wa kuzungumza. Habwe na Karanja (2004), wakimnukuu Omondi (1994), wanaeleza maana ya ugeuzaji kuwa ni utaratibu wa sarufi ambaao unapotekelezwa kwenye mfululizo wa ishara za kileksika katika mfumo fulani, unatoa athari fulani. Wanaendelea kueleza kuwa sarufi geuzaji hueleza ujuzi wa lugha ambaao msemaji mzawa anao na unamwezesha kutunga sentensi sahihi. Utafiti huu unaangalia kanuni geuzaji kama mfumo wa sheria unaotumiwa kuzalisha sentensi zenye maumbo anuwai zinazowakilisha dhana sawa kutokana na sentensi ya kimsingi. Tazama mifano ifuatayo:

1. a) Mwalimu amempa mwanafunzi zawadi.
b) Mwanafunzi amepewa zawadi na mwalimu.
2. a) Mtoto atapeleka barua kwa babake.
b) Mtoto atampelekea babake barua.

Mifano ya sentensi namba 1 na 2 hapo juu inaonesha uamilifu wa kanuni geuzaji katika kuzalisha sentensi za kimsingi na nyingine za ziada. Sentensi 1 (a) na 2 (a) ni za kimsingi zilizohusisha matumizi ya vitenzi ‘pa’ na ‘peleka’ katika kauli ya kutenda mtawalia. Katika sentensi hizi, viima ‘mwalimu’ katika sentensi 1 (a) na ‘mtoto’ katika sentensi 2 (a) vimejitokeza katika nafasi yake kwenye Kundi Nomino huku yambwa ‘mwanafunzi’ na ‘barua’ zikijitokeza kwenye Kundi Tenzi mtawalia. Sentensi 1(b) na 2 (b) zinawakilisha tungo za ziada ambazo umilisi wa mzawa za lugha humwezesha kutunga. Katika sentensi hizi, kitenzi ‘pa’ kimenyambuliwa katika kauli ya kutendewa huku kitenzi ‘peleka’ kikinyambuliwa katika kauli ya kutendeka. Kadhalika, nafasi za kiima na yambwa zimebadilika. Licha ya sentensi hizi kuwa na maumbo tofauti, zinawakilisha dhana sawa.

Kwa upande mwingine, Matinde (2012) anaeleza ugeuzaji kama utaratibu unaotumiwa katika Sarufi Geuza Miundo Zalishi kubadili umbo la tungo kuwa umbo jingine na wakati uleule huzalisha sentensi lukuki kwa kutumia kanuni mahususi na ujuzi wa lugha alionao msemaji mzawa. Kwa mujibu wa TUKI (1990), nadharia hii ya sarufi inatilia uzito uwezo wa kanuni chache za kisarufi kuzalisha au kuunda sentensi nyingi zenye urefu usio na kikomo, na zenye uhusiano kati ya maumbo yake ya ndani na nje.

Sentensi zinazozalishwa katika lugha huwa na umbo moja la ndani (Massamba na wenzake, 1999). Kanuni geuzaji hutumika kuyageuza maumbo hayo ya ndani ili kupata maumbo tofauti ya nje ambayo ndiyo yanajitokeza katika usemajii. Kwa hiyo, kanuni geuzaji hutumika kuonesha uhusiano uliopo kati ya maumbo mbalimbali ya tungo na vilevile uhusiano unaoweza kuwapo baina ya tungo ambazo zina umbo la nje tofauti lakini umbo la ndani lililo sawa.

Massamba (2004) anaeleza umbo la ndani kama umbo la kirai, sentensi au tungo yoyote ambalo huwa kiini cha usemajii unaojitokeza nje baada ya kufanyiwa mabadiliko kadhaa. Kulingana na TUKI (1990), umbo la ndani ni mshikamano dhahania wa vipashio vya tungo ambaao ndio msingi wa fasili ya maana kamili ya sentensi. Umbo hili hujitokeza katika sentensi kabla ya sentensi hiyo kufanyiwa mageuzi yoyote na ndilo linalobeba maana kamili ya tungo. Umbo hili huwa si sahihi katika usemajii kama inavyodhahirika katika mifano ifuatayo:

3. Mama pika wali jioni.
4. Mabawabu linda lango jana usiku.

Kwa mujibu wa Massamba (2004), umbo la nje hutokea pale umbo ndani linapofanyiwa mageuzi yanayohitajika hadi kufikia kiwango cha usemajii unaokubalika. Matinde (2012) anafafanua zaidi kuwa mageuzi haya hujumuisha uambishaji wa viambishi mbalimbali vyenye uamilifu wa kisarufi. Maelezo haya yana maana kuwa umbo la nje hudhihirika kimatamshi na kiothografia. Mifano:

5. Mama *atapika* wali jioni.
6. Mabawabu *walilinda* lango jana usiku.

Usemajii unaokubalika na kudhihirika katika umbo la nje umetokana na mageuzi yaliyohusu uambishaji wa viambishi vya nafsi {*a*} katika ‘{*a*}tapika’ na {*wa*} katika ‘{*wa*}lilinda’ na viambishi vya njeo {*ta*} katika ‘a{*ta*}pika na {*li*} katika ‘wa{*li*}linda’.

Ugeuzaji unaweza kufanywa kuitia mbinu kama vile udondoshaji, uchopекаji, upanguaji, ubadilishaji wa nafasi ya yambwa, ugeuzaji masharti, ugeuzaji kanushi na ugeuzaji swalifu (Massamba na wenzake, 1999; Matinde, 2012). Kuitia njia hizi, sifa kuu ya nadharia geuzaji ambayo ni uwezo wa sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizoweza kuhesabika katika lugha kutokana na umilisi mpana wa mzawa wa lugha, hubainika.

Lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha nyingine duniani, ina namna ya kupanga vipashio vyake ili kuunda sentensi au matini zenye maana. Sintaksia inajitokeza kama mojawapo ya tanzu za kiisimu inayoweka kanuni za upangaji wa vipashio vya lugha katika sentensi. Upangaji huu hufanywa kwa njia inayozingatia userifu na ukubalifu wa sentensi pamoja na mshikamano katika kauli ndefu.

Kwa kawaida, sentensi za Kiswahili huwa na mfuatano wa vipashio ambapo Kundi Nomino (KN) hutangulia Kundi Tenzi (KT). Katika utaratibu huu, KN huchukua uamilifu wa kiima huku KT likichukua uamilifu wa kiarifu. Hata hivyo, kutokana na sheria geuzaji, mpangilio wa vipashio katika sentensi huweza kugeuzwa ili kuzalisha sentensi nyingine. Matini za utangazaji wa mchezo wa kandanda hubainisha Kanuni Geuzaji kuitopia upanguaji, uchopekaji/ugeuzaji wa kauli tendwa, udondoshaji na ubadilishaji wa nafasi ya yambwa.

4.1.1 Upanguaji

Hii ni aina ya ugeuzaji ambapo panatokea ubadilishaji wa nafasi za elementi katika tungo (Habwe na Karanja, 2004). Hii inamaanisha kuwa viambahengo vya tungo hukaa mahali ambapo kwa kawaida si pake katika sentensi. Mifano ya upanguaji iliyojitokeza katika data ya utafiti huu ni pamoja na:

7. *Upesi upesi anarudi nyuma difenda kuokoa ule mpira* badala ya ‘Difenda anarudi nyuma upesi upesi kuokoa mpira ule.’
8. *Anatoa ile pasi Rooney kwake Valencia* badala ya ‘Rooney anatoa pasi ile kwake Valencia.’
9. *Ile kona itachezwa kuelekea lango la ulinzi* badala ya ‘Kona ile itachezwa kuelekea lango la ulinzi.’
10. *Anaingia pale kwenye eneo la hatari mchezaji Wanga* badala ya ‘Mchezaji Wanga anaingia pale katika eneo la hatari.’
11. ...*anakwenda na mpira mshambulizi huyu van Persie, anacheka na wavu msikilizaji* badala ya ‘Msikilizaji mshambulizi huyu van Persie anakwenda na mpira, anacheka na wavu.’

Chanzo: Matangazo ya Mchezo wa Kandanda kutoka Vituo vya Redio na Runinga

Kutokana na upanguaji huu, chagizo ‘upesi upesi’ katika matini ya 7 kinetangulia kiarifu ‘rudi’ huku kiarifu ‘rudi’ kikitangulia kiima ‘difenda.’ Hali hii inajitokeza pia katika matini ya 8 na 9 ambapo kivumishi ‘ile’ kinatangulia nomino ‘pasi’ na ‘Rooney’ huku kivumishi ‘ile’ kikitangulia nomino ‘kona’ mtawalia. Katika matini ya 10, kiima ‘mchezaji Wanga’ inatanguliwa na kiarifu ‘anaingia pale’. Hali hii inajitokeza pia katika matini ya 11 ambapo kiima ‘mshambulizi huyu van Persie’ kinatanguliwa na kiarifu ‘anakwenda na mpira.’

Katika data hiyo, matini zilizo katika hatimlazo ziko katika umbo la nje na zile zilizo katika alama za mtajo ziko katika umbo la ndani. Licha ya kuonesha uhalisi wa lugha ya maongezi ya kawaida ambapo wakati mwingine wazungumzaji hawawi makini kuzingatia kanuni za kisintaksia, upanguaji hubainisha pia uwezo

wa mtumiaji wa lugha kuzua matini nyingi zenyenye kuwasilisha dhana sawia na hivyo kurahisisha mawasiliano.

4.1.2 Uchopekaji/Ugeuzaji wa Kauli Tendwa

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza uchopekaji kuwa ni uingizaji wa elementi katika tungo hasa pale sentensi ya kauli ya kutenda inapogeuzwa kuwa sentensi ya kauli ya kutendwa. Kulingana na utafiti huu, kihuishi ‘na’ ndicho kipashio kinachochopekwa. Uchanganuzi wa matini zifuatazo unaonesha ugeuzi huu:

12. *Yule difenda anachengwa na mshambuliaji matata badala ya ‘Mshambuliaji matata anamchenga difenda yule.’*
13. *Timu ya Thika United imefungwa mabao matatu kwa moja na timu ya Tusker* badala ya ‘Timu ya Tusker imeifunga timu ya Thika United mabao matatu kwa moja.’
14. *Anatiliwa pasi nzuri pale Sserenkuma, anakwenda, anakwenda, anaingia ndani ya boksi, analazwa chini na Situma* badala ya ‘Anatiliwa pasi nzuri pale Sserenkuma, anakwenda, anakwenda, anaingia ndani ya boksi na Situma anamlaza chini.’
15. *Mchezo unamalizika msikilizaji, mabingwa watetezi Gor wamekaangwa na limbukeni hawa Nakuru Top Fry* badala ya ‘Mchezo unamalizika msikilizaji, limbukeni hawa Nakuru Top Fry wanawakaanga mabingwa watetezi Gor Mahia.’

Chanzo: Matangazo ya Mchezo wa Kandanda kutoka Vituo vya Redio na Runinga

Katika mpangilio wa kawaida wa vipashio vya lugha katika sentensi ya Kiswahili, kitenda au kiwakilishi chake (KN_1) hutangulia kitendwa (KN_2). Hata hivyo, matini hizi zinaonesha kuwa nafasi ya KN_1 na KN_2 zinabadilika. KN_2 linalobeba vitendwa ‘Yule difenda’, ‘Timu ya Thika United’ na ‘Sserenkuma’ vinatangulia KN_1 linalosheheni vitenda ‘Mshambulizi matata’, ‘Timu ya Tusker’ na ‘Situma’ katika matini ya 12, 13 na 14 mtawalia. Ugeuzaji wa namna hii umedhihirisha mnyambuliko wa vitenzi ‘chenga’, ‘funga’ na ‘lala’ kutoka kauli ya kutenda hadi ya kutendwa. Hali hii ndiyo inayodhahirika pia katika matini ya 15 ambapo kitenzi ‘kaanga’ kinanyambuliwa katika kauli ya kutendwa mtawalia.

Hali hii inatokana na uchopekaji wa mofimu {w} kama kiambishi kifuatilizi pamoja na kihuishi *na* katika sentensi. Katika mpangilio huu, umbo nje ndilo linalodhahirika kimatamshi. Kwa mfano, katika matini ya 16, umbo la ndani ni ‘Timu ya Tusker imeifunga timu ya Thika United mabao matatu kwa moja’ huku umbo la nje likiwa ‘Timu ya Thika United imefungwa mabao matatu kwa moja na timu ya Tusker’. Ruwaza hii inajitokeza pia katika matini ya 15, 17, 18, na 19 ambapo sentensi zilizo katika umbo la ndani zimeoneshwa kwa alama za mtajo na zile zilizo katika umbo la nje zimeandikwa kwa hatimlazo. Huku umbo la ndani

likiwa S \longrightarrow KN₁ + KT (tenda) + KN₂, umbo nje huwa S \longrightarrow KN₂ + KT (tendwa) + KN₁. Ugeuzaji huu wa vipashio katika sentensi unadhihirika kama njia mojawapo inayotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda kuunda matini zinazowasilisha ujumbe kwa njia angavu zaidi ambayo wakati mwingine hujitokeza katika lugha ya maongezi.

4.1.3 Udondoshaji

Kwa mujibu wa Njogu na wenzake (2006), udondoshaji ni uondoaji wa baadhi ya vipashio vyta sentensi kwenye matini. Kulingana na maelezo haya, kauli zinazotokana na mchakato wa udondoshaji huwa hazikamiliki. Hata hivyo, licha ya msemaji kujieleza kwa kutumia maneno machache kutokana na kudondolewa kwa baadhi ya maneno au vipashio, ujumbe bado humfikia mlengwa kwa ukamilifu. Habwe na Karanja (2004) na Massamba (2004) wanaafikiana kuwa udondoshaji ni ugeuzaji unaohusisha kuondolewa kwa baadhi ya viambajengo vyta sentensi katika silabi, neno, kirai au kishazi. Wataalamu hawa wanaendelea kusema kuwa udondoshaji hufanya sentensi kuwa fupi kuliko inavyopaswa kuwa na hivyo kumwezesha msemaji kudokeza maneno machache tu huku akimaanisha zaidi ya kile anachosema. Matini zifuatazo zilijitokeza katika data ya utafiti huu zikibainisha udondoshaji:

16. Anamegewa pasi ya mwaka pale na kutuliza. Anakwenda na mpira, anakwenda nao, (mpira), anakwenda (na mpira) anapiga (mpira lakini unatoka) nje.
17. Wanaanza mpira Sofapaka, wanakwenda mbele, wanakwenda (mbele), hatari katika lango, hatari pale (katika lango), hatari... (katika lango).
18. Mechi inakaribia kuanza hapa Anfield. Kumbuka kwamba timu hizi mbili zinatengwa na alama tano tu. Liverpool wakiwacharaza Chelsea watabeba (kombe/taji), lakini vijana hawa wa Mourinho wakirarua Liverpool wana nafasi (ya kushindania taji).
19. Anachenga pale moja Suarez, (anachenga ya) pili, (anachenga ya) tatu, anaachilia (kombora) goo-ooool!
20. Naona hapa (timu ya) AFC Leopards imetiwa mkononi na (timu ya) Sofapaka, imeshatandikwa hapa (goli) mbili (kwa) nunge.

Chanzo: Matangazo ya Mchezo wa Kandanda kutoka Vituo vyta Redio na Runinga

Maneno yaliyoko kwenye mabano ni yale yanayopaswa kutamkwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda katika mfululizo lakini hayatamkwi, yaani yanadondoshwa. Hata hivyo, watangazaji wa mpira wanachukulia kuwa wanaeleweka kwa wasikilizaji wao kwa maneno hayo machache. Umbo la ndani la matini hizi linawakilishwa na maneno yaliyoandikwa katika mabano, yaani ‘Anachenga pale moja Suarez, (anachenga ya) pili, (anachenga ya) tatu, anaachilia

(kombora) goo-ool!’ katika matini ya 19. Umbo nje linalodhahirika katika usemajি nalo linawakilishwa na matini zisizo na maneno yaliyoandikwa katika mabano, yaani ‘Anachenga pale moja Suarez, pili, tatu, anaachilia goo-ool!’ Umbo ndani linadhihirika pia kwa kujumuisha maneno yaliyo katika mabano katika matini 16, 17, 19 na 20 huku umbo la nje likiwakilishwa pasipo kujumuisha maneno yaliyo katika mabano kwenye matini hizo. Matini hizi zinaonesha kuwa maneno yaliyo katika mabano ambayo hayatamkwii yalikwishatamkwa awali au si lazima yarudiwe kwa kuwa ujumbe umekwshawafikia wasikilizaji. Inajitokeza kuwa umbo la nje linadhihirisha utoshelevu wa kipragmatiki.

Udondoshaji umedhahirika pia kupitia matumizi ya viunganishi. Kapinga (1983) anaeleza viunganishi kama aina mojawapo ya maneno yanayoleta pamoja na kuonesha uhusiano baina ya neno na neno au fungu moja la maneno na jingine. Viunganishi huwa na dhima ya kuleta vipashio vya lugha pamoja (Mgullu, 1999). Kupitia uunganishi, vipashio vya lugha vinavyohusika huwa na mshikamano unaodhahirika kupitia muumano wa vijenzi vya sentensi. Viunganishi hutumiwa kama daraja hivi kwamba vikikosekana basi mshikamano wa matini na uyakinifu wa ujumbe haujitokezi kikamilifu. Kulingana na utafiti huu, matumizi ya viunganishi yamesababisha udondoshaji wa baadhi ya nomino katika matini za mchezo wa kandanda. Tazama mifano ifuatayo:

21. Mpendwa msikilizaji popote ulipo tunakukaribisha katika dimba hili la leo. Hii ni **mechi** kali inayotazamiwa kuwa ngumu sana *kwa sababu* inahusu **timu** mbili hasimu tangu jadi *na* zinazotazamia kunyakua taji la ligi msimu huu.
22. Mara ya mwisho timu hizi maadui zilipokutana ziliweza kufanya ukatili wa kuumiza nyasi bure kwa kutoka suluhu bin suluhu, sijui leo **mambo** yatakuwa vilevile *au* vipi. **Malango** yote mawili ya timu hizi maarufu yalilalamika *kwa sababu* ya kulazwa njaa, tusubiri tuone kama leo yatalishwa.
23. **Timu** zote mbili zinajivunia ubingwa wa miaka ya nyuma *na* wachezaji wakali waliosifika sana katika ligi hii na kanda yote ya Afrika Mashariki na Kati. Naona zimejinoa hapa katika harakati zao za kuendeleza ubabe wao. **Chanzo:** Matangazo ya Mchezo wa Kandanda kutoka Vituo vya Redio na Runinga

Ugeuzaji unganishi huweka pamoja sentensi zenye maumbo au vipashio sawa na kuunda sentensi moja inayowakilisha maana iliyokusudiwa. Aina hii ya ugeuzaji hudhamiria kuepuka kurudia vipashio vya lugha hasa nomino na kitende vinavyotokea mara kadhaa katika matini kwa kuvidondosha. Katika matini zilizoonyeshwa hapo juu, matumizi ya kiunganishi ‘*kwa sababu*’ yanaepusha hali

ya kurudia nomino ‘mechi’ katika matini ya 21 na nomino ‘malango’ katika matini ya 22. Matini hizi zinawakilisha umbo la nje. Kwa ukamilifu wake, sehemu hii ya matini ya 21 ingesomeka hivi ‘...Hii ni **mechi** kali inayotazamiwa kuwa ngumu sana *kwa sababu mechi* hii inahusu timu mbili hasimu tangu jadi...’ Matini ya 22 ingesomeka ‘...**Malango** yote mawili ya timu hizi maarufu yalilalamika *kwa sababu ya malango* kulazwa njaa...’ ili kuwakilisha umbo la ndani. Kadhalika, kiunganishi ‘na’ kimemwepushia mtangazaji haja ya kurudia nomino ‘timu’ katika matini ya 23. Kwa upande mwingine, inatokea kuwa hamna haja ya kurudia nomino ‘mambo’ kutohana na kuwapo kwa kiunganishi ‘au’ katika matini ya 22.

Udondoshaji huu hutokana na hali ya watangazaji kutotaka kurudia maneno yasiyo muhimu katika ufikishaji wa ujumbe, hasa baada ya kuyataja mwanzoni wanapotangaza. Hii ina maana kuwa udondoshaji huyafanya maongezi kuepuka matumizi ya maneno ambayo yanajulikana kwa msemaji/mtangazaji na msikilizaji/shabiki katika muktadha ambamo usemi unatumwiwa. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa wasemaji hudokeza maneno machache tu huku wakimaanisha zaidi ya kile wanachosema. Watangazaji wa mpira wanachukulia kuwa kwa kutorudia maneno hayo ambayo wamekwishayataja mwanzoni, wanaeleweka kwa wasikilizaji wao na hivyo kufikisha ujumbe.

Kadhalika, udondoshaji unaotokea katika lugha ya utangazaji huweza kusababishwa na kasi ya mchezo wenyewe na muda mchache walionao watangazaji ambao hauwaruhusu kutaja maneno yote na baadhi ya majina ya wachezaji katika kueleza mfululizo wa matukio ya mchezo. Kwa hiyo, matumizi ya maneno machache huwa na uamilifu wa kumwezesha mtangazaji kuhimili kasi na mfululizo wa mchezo wa kandanda anapotangaza. Hata hivyo, watangazaji wanatarajia kuwa wasikilizaji wao ambao pia ni mashabiki wa mchezo huu huelewa maana ya kauli hizi zilizodondoshwa kwa sababu wanang’ amua miktadha ya kipragmatiki ambayo zimetumiwa.

4.1.4 Ugeuzaji Unaobadilisha Nafasi ya Yambwa

Ugeuzaji wa aina hii hutumika katika sentensi zenyenitenzi elekezi (Massamba na wenzake, 1999). Sentensi hukamilika tu pale ambapo yambwa inajitokeza katika matini. Kwa hiyo, tungo zinazozalishwa hudhahirisha hali ya kubadilishwa kwa nafasi ya yambwa. Ifuatayo ni mifano ya matini za sajili ya mchezo wa kandanda zilizotokana na data ya utafiti huu:

24. *Wanasonga na mpira pale katikati ya uwanja, anachukua Rooney, anaangaliaacheze wapi, anacheza mpira kwa Valencia* badala ya ‘Wanasonga na mpira pale katikati ya uwanja, anachukua Rooney, anaangaliaacheze wapi, anamchezea Valencia mpira’.

25. *Sikiliza kona hii kwa makini msikilizaji. Anachanja pale kona kwa nani yule-ee Sturridge* badala ya ‘Sikiliza kona hii kwa makini msikilizaji. Anamchanja Sturridge.
26. ...*wanakwenda kasi, wanakwenda Manchester, anamega pasi ile kwake Carrick* badala ya ‘...wanakwenda kasi, wanakwenda Manchester, anammegea Carrick pasi ile.’

Chanzo: Matangazo ya Mchezo wa Kandanda kutoka Vituo vya Redio na Runinga

Sentensi hizi zimepitia ugeuzaji unaobadilisha nafasi ya yambwa. Yambwa tendwa katika matini hizi (mpira, kona na pasi) ambayo kwa kawaida hutokea baada ya yambwa tendewa (Valencia, Sturridge na Carrick) sasa zinajitokeza mwanzo. Katika usemaji wa kawaida, yambwa zingejitokeza katika nafasi zake kwa kuchopeka kiambishi {m} cha yambwa katika vitenzi husika huku vitenzi hivyo vikinyambuliwa katika kauli ya kutendea ili kupata ‘anamchezea’ katika matini ya 24, ‘anamchanja’ katika matini ya 25 na ‘anammegea’ katika matini ya 26. Hali hii ya kubadilisha nafasi ya yambwa kuititia kauli ya kutendea ina dhima ya kutambilisha mchezaji anayemiliki mchezo kwa wakati fulani maalumu na kuwakilisha umbo la ndani katika matini hizo.

Matini hizi zinadhishirisha Kanuni Geuzaji kuititia upanguaji, uchopekaji, udondoshaji na ugeuzaji unaobadilisha nafasi ya yambwa. Ubadilishaji huo hubainisha sifa kuu ya kanuni geuzaji ambayo ni uwezo wa sheria chache kuzalisha sentensi nyingi zisizoweza kuhesabika katika lugha kutokana na umilisi wa mzawa wa lugha na ambazo zina uamilifu wa kimawasiliano (Chomsky, 1965).

4.1.5 Uwakilishi Rejeleaji

Uwakilishaji ni dhana inayotumiwa katika isimu kumaanisha vipashio vya lugha vinavyosimamia vile visivyotajwa katika matini. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), viwakilishi ni maneno ambayo hutumiwa badala ya nomino na kwamba nomino zinazowakilishwa huwa hazitajwi. Kirejeshi nacho ni neno au kiambishi katika neno kinachohusishwa na jambo fulani lililotajwa awali. Hivyo basi, uwakilishi rejeleaji hujitokeza kama neno au kiambishi kinachowakilisha jambo lililokwishatajwa awali. Wanaoweza kurejelewa katika sajili ya mchezo wa kandanda kutokana na lugha ya utangazaji ni wachezaji na watangazaji. Data ya utafiti huu ilibainisha uwakilishaji huu kama ifuatavyo:

27. ...*mchezaji huyu anaonyesha kuwa yeye si mchache, anamdhishirisha kocha wake kwamba alifanya busara kumchezeshwa.*
28. Naona wachezaji wa timu ya Sofapaka *wanarejea uwanjani na kujipanga* katika nafasi zao, ishara kuwa *wao wako tayari kumenyana tena na wenzao* katika kipindi hiki cha pili kitakachoanza wakati wowote kutoka sasa.

29. ...Anachanja pale-ee go-goo-ooo! Anasherehekea kwa *kujipiga* kifua na *kujiambia* kuwa *yeye* ndiye dume wa kufanya mambo.
30. Waliokuleteeni matangazo haya ya kabumbu ni *sisi* watangazaji wenu Ali Salim Manga na Jack Oyoo. *Tukutane* tena uwanjani siku nyingine, *tunasema* kwaherini.
- Chanzo:** Matangazo ya Mchezo wa Kandanda kutoka Vituo vya Redio na Rusinga

Katika matini ya 27, kipande ‘yeye si mchache’ ni urejeshi. Kinachorejelewa na kuwakilishwa na ‘yeye’ ndicho kinachorejelewa na kiambishi *{a}* katika *{a}*namdhahirisha kinachowakilisha nafsi ya tatu umoja. Kadhalika, kinachorejelewa na ‘wao’ katika matini ya 28 ndicho kinachowakilishwa na kiambishi *{wa}* katika *{wa}*narejea cha nafsi ya tatu wingi. Virejelewa katika matini hizi ni mshambulizi na wachezaji, mtawalia. Kulingana na matini ya 29, kiwakilishi ‘yeye’ na kiambishi *{a}* katika *{a}*nasherehekea na katika *{a}*nachanja vinarejelea mchezaji anayewakilishwa na nafsi ya tatu umoja. Katika matini ya 30, ‘Sisi’ ni kiambishi cha nafsi ya kwanza umoja kinachowakilishwa na kiambishi *{tu}* katika *{tu}*kutane na *{tu}*nasema. Kiambishi hiki kinarejelea watangazaji wa mchezo walijotajwa.

Urejeleaji hutokea pia pale ambapo katika sentensi, mtu aliyetajwa anajitendea jambo mwenyewe. Urejeleaji huu umebainika kupitia uambishaji wa kiambishi *{ji}* katika kitenzi ili kupata ‘*kujipanga*’ katika matini ya 28 na vilevile ili kupata ‘*kujipiga*’ na ‘*kujiambia*’ katika matini ya 29. Massamba na wenzake (1999) wanasema kuwa kauli ya kujirejelea huhusu uhusiano wa kitenzi na kiima tu bila kuhusisha yambwa. Wanaeleza zaidi kuwa katika kauli hii, mtenda na mtendwa (au lengo) ni kitu kilekile; yaani mtenda hujitenda au hujitendea yeye mwenyewe. Matini zifuatazo ni mifano zaidi ya kuwapo kwa ujirejeleaji katika matangazo ya mpira.

31. ...Suarez anachezewa visivyo katika eneo la hatari na anajirusha ndani ya kisanduku kile. Refa anasema si penalti.
32. Mchezaji huyu wa kiungo anajizoazoa pale katikati ya uwanja baada ya kupata chenga ya maudhi kutoka kwa kiungo machachari Ozil.
33. ...anakwenda pale-eee, analishwa kiatu. Naona mshambuliaji huyu ameshambuliwa hapa. Anagaragara pale na *kujishashasha* chini.

Matini zilizonakiliwa hapo juu (31, 32 na 33) zinaonesha kuwa mtenda ametenda jambo kuhusiana na yeye mwenyewe. Kirejeaji *{ji}* kimetumiwa kuonesha hali ya kutorudia usemi. Kwa jumla, urejeleaji hudhihirika kama kipengele cha sarufi geuzaji kinachotumika sana katika muundo wa matini kuleta muwala na uhalisi katika usemi. Vilevile, urejeshi huwa na dhima ya kusisitiza ujumbe ili kueleweka

zaidi kwa wasikilizaji kutokana na kauli kuwa viwakilishi hivi vinadokeza dhana sawa.

5.0 Hitimisho

Makala hii imechanganua matini zinazotumiwa katika sajili ya mchezo wa kandanda ili kufuma maana matinishi. Uchanganuzi huu umebainisha kuwa upangilifu wa vipashio vya lugha kwa mujibu wa kanuni zilizokubalika hujenga tungo zenye maana matinishi. Maana matinishi imetumikisha kanuni za kisarufi na kusarufi ujumbe kutokana na kanuni geuzaji za upanguaji, uchopekaji, udondoshaji, ugeuzaji unaobadilisha nafasi ya yambwa na uwakilishi rejeleaji. Licha ya kuonesha uhalisi wa lugha ya maongezi ya kawaida, aina hizi za ugeuzaji huwawezesha watangazaji wa mchezo wa kandanda kutumia lugha kwa njia inayozalisha matini nyingi zenye dhana sawia ili kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji kwa njia bora zaidi bila kurudia baadhi ya vipashio vinavyooleweka kwao wote.

Aidha, sifa hizi za kanuni geuzaji zimebainisha maana matinishi kutokana na muwala na msisitizo wa ujumbe katika usemi. Pamoja na haya, sifa hizi zimewezesha kuunganishwa kwa vipashio vya lugha ili kuunda matini zenye mshikamano kwa njia inayowasaidia wasikilizaji kufuatilia matukio na mkondo wa mchezo kwa urahisi na hivyo kufanikisha mawasiliano. Kwa ujumla, uchanganuzi wa matini zilizotokana na kauli za matangazo katika sajili ya mchezo wa kandanda umeweza kubainisha lugha kama mfumo wenye maana matinishi.

Marejeleo

- Bolinger, D. and Sears, D. (1981). *Aspects of Language*. (3rd edition). New York: Harcourt Brace Javanorich Inc.
- Caffarel, A. (2010). "Systemic Functional Grammar and the Study of Meaning". In Narrog, H. and Heine, B. (Eds.). *The Oxford Handbook of Linguistic Analysis*. New York: Oxford University Press. pp. 883-984.
- Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures*. Berlin: Walter de Gruyter.
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge, MA: MIT Press.
- Cook, A. B. (1969). *Introduction to English Language: Structure and History*. New York: The Ronald Press Company.
- Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Halliday, M. A. K. (2004, 1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.
- Halliday, M. A. K. and Hasan, R. (1989). *Language, Context and Text: Aspects of Language in a Social-Semiotic Perspective*. Oxford: Oxford University Press.
- Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

- Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. (2nd edition). New Delhi: New Age International Publishers.
- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA): *Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mwinlaam, I. N and Winfred, W. X. (2016). A Survey of Studies in Systematic Functional Language Description and Typology, *Functional Linguistics*. 3(8):1-41.
- Njogu, K., Mwiaki, A. na Buliba, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili: Uchanganuzi na Matumizi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- TUKI (1990). *Kamusi ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.